# Fomula ya Tamthiliya ndani ya Tamthiliya katika Tamthiliya Teule za Kiswahili

*A. Mnenuka*

*Ikisiri*

Upekee wa mwandishi katika kazi za fasihi si suala geni miongoni mwa wanazuoni wa fasihi. Mwandishi wa kazi za fasihi ana uhuru wa kutumia mbinu yoyote ya kisanaa ili kujenga uwiano mzuri wa fani na maudhui. Makala haya yanachunguza mbinu iliyojitokeza katika baadhi ya kazi za tamthiliya teule za Kiswahili. Mbinu hii ni ile ya kutumia mchezo wa kuigiza ndani ya tamthiliya. Katika makala haya tunachunguza mbinu hiyo na kuonyesha kwa ukaribu uhusiano wake na maudhui ya tamthiliya nzima. Aidha, makala haya yanajadili uhusiano wa kimaudhui uliopo baina ya michezo hiyo ya kuigiza katika tamthiliya inayohusika na sehemu nyingine ya tamthiliya, uhusiano ambao tumeupa jina la 'sauti na mwangwi' kwa mujibu wa fasili na ufafanuzi wa kifizikia wa dhana hizo mbili.

## 1.0 Utangulizi

Mtindo unaotumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ndio unaompa upekee baina yake na waandishi wengine. Kwa hakika, ndio hasa msingi wa utajiri wa sanaa – uzuri unaojitokeza katika umbo sanifu. Wasanii wa fasihi ya Kiswahili, kama ilivyo kwa wasanii wengine, wameonesha ubunifu wa hali ya juu katika sanaa. Ubunifu wao unajitokeza katika tamthiliya za Ebrahim Hussein na Penina Mlama katika tamthiliya za *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi* na *Lina Ubani* kwa mfuatano huohuo. Unajitokeza pia katika Ushairi na baadhi ya riwaya za Euphraze Kezilahabi kama *Kichomi, Karibu Ndani, Nagona* na *Mzingile.* Kazi za Mulokozi na Kahigi kama *Ushairi na Kunga za Fasihi* na *Malenga wa Bara* ni kazi nyingine zenye sanaa ya kipekee katika fasihi ya Kiswahili (Senkoro, 2006).

Makala haya yanalenga kuchunguza matumizi ya Fomula ya Tamthiliya ndani ya Tamthiliya (FTT) kama mbinu au mtindo utumiwao na waandishi katika kusisitiza maudhui ndani ya tamthiliya teule. Tamthiliya zilizoteuliwa ni *Mashetani* ya Ebrahim Hussein (1971), *Giza Limeingia* ya Emmanuel Mbogo (1977), na *Kaptula la Marx* ya Euphraze Kezilahabi (1989). Katika sehemu inayofuata kuna ufafanuzi wa baadhi ya dhana muhimu zitakazotumiwa katika makala haya. Baadhi ya dhana hizo ni mchomozo, maigizo, mchezo wa kuigiza na tamthiliya.

### 1.1 Ufafanuzi wa Dhana

Dhana ya tamthiliya imefafanuliwa kuwa ni "… utungo wa drama…" (Mlama, 1983:206). Hivyo, tamthiliya ni maandishi ambayo yanaweza kutendwa jukwaani kama drama. Dhana hii ya tamthiliya ndio itatumika katika makala haya badala ya ile iliyotolewa na Mulokozi (1996) kuwa tamthiliya, drama na

mchezo wa kuigiza ni kitu kimoja. Tunapendekeza kuwa dhana ya tamthiliya ibaki kuwa maandishi yanayoweza kutendwa jukwaani kama drama au mchezo wa kuigiza au igizo kama inavyojulikana katika lugha ya kawaida. Maandishi ya mchezo yaitwe "tamthiliya" na maandishi hayo yakitendwa jukwaani yaitwe drama kama Wamitila (2003) anavyobainisha. Kwa kuwa maandishi na utendaji ni vitu viwili tofauti na vyenye msukumo na mbinu tofauti katika kuelezea maudhui ya kazi ya fasihi, ni vema utofauti huo ujitokeze pia katika istilahi zinazotumika. Kutokana na hoja hiyo, drama za kimiviga haziwezi kuitwa tamthiliya kwa sababu hazikuanza kuandikwa wala kuwasilishwa au kusomwa kibinafsi katika maandishi.

Mchomozo kwa upande mwingine ni hali ya kupachika elementi mpya katika elementi nyingine zinazofanya kazi katika ruwaza ya sentensi na kama zinavyoweza kueleweka kwa msomaji au msikilizaji (Van Peer na Hakemulder, 2006). Kwa mujibu wa Van Peer na Hakemulder (weshatajwa), kuna ala mbili za mchomozo ambazo ni ukengeushi na usambamba. Dhana ya mchomozo, iliasisiwa na Šklovskij na baadaye kuboreshwa na Jan Mukařovský, na kuelezwa kuwa ni uwekaji wa miundo, matendo na vitu vingine visivyozoeleka kinyume na mazoea ya hadhira, na vinaweza kuoneshwa kisaikolojia, kitamaduni na kiisimu. Ala hizi hazitumiki kwa malengo ya kupamba tu kazi ya kifasihi bali kwa malengo maalumu kama wasemavyo Shklovsky na Wanaurasimi wengine (Van Peer na Hakemulder, 2006). Kwa kuzingatia maelekezo hayohayo, mchomozo katika makala haya ni utumiaji wa miundo isiyozoeleka katika kazi hiyo ya fasihi ili kuleta athari kwa msikilizaji au msomaji wa kazi hiyo. Miundo inayorejelewa hapa ni utumiaji wa mbinu ya tamthiliya ndani ya tamthiliya kwa malengo maalumu.

Aidha, *Sauti* na *Mwangwi* ni dhana mbili zinazokaribiana sana kimaana na kimatumizi katika mawasiliano ya kawaida ya lugha. *Sauti* katika mazingira ya kawaida ni mlio wowote unaoweza kusikika. Aghalabu mlio huo unaweza kutokana na mgongano, msuguano wa vitu, au kutoka katika kinywa au kinyo cha wanyama. *Mwangwi* ni sauti inayosikika kwa mara nyingine baada ya mawimbi ya sauti kugonga na kuakisiwa katika pango, bonde au msitu. Kwa mantiki hiyo, kuna uwezekano wa kuwa na sauti bila mwangi, lakini hakuna uwezekano wa kuwa na mwangwi bila sauti. Katika makala haya tutazitumia dhana hizi mbili kwa kuhusisha na sehemu za tamthiliya teule, ambapo sehemu nyingine zitaitwa sauti na nyingine zitaitwa *mwangwi*. Sauti ni ile sehemu ambayo inazungumzia wazo kuu au wazo-kiini katika tamthiliya, wazo ambalo linafafanuliwa zaidi kwa kutumia mifano kadha wa kadha, kama mwangwi, katika sehemu nyingine za tamthiliya. Tunaamini kuwa iwapo msomaji wa tamthiliya anasoma kwa makini *sauti* au mchezo ndani ya *tamthiliya* anaweza

kupata wazo kuu bila kusoma sehemu ya tamthiliya iliyosalia ambayo inaelezea kitu kilekile kwa mifano mbalimbali.

## 2.0 Tamthiliya ndani ya Tamthiliya

Tamthiliya ndani ya Tamthiliya ni maandishi ya kidrama ambapo mwandishi wa tamthiliya anawavalisha uhusika mwingine wa kisanaa wahusika wa tamthiliya na kuwapa nafasi ya kuigiza mchezo mwingine ndani ya tamthiliya. Utokeaji huo huitwa mchomozo katika tamthiliya kwa sababu matarajio ya wengi katika tamthiliya ni kuona visa katika dunia halisi ya wahusika na sio dunia ya kubuni. Fomula hii haikuanza kutumiwa na waandishi wa tamthiliya ya Kiswahili tu bali imetumiwa kwa miaka mingi tangu enzi za Thomas Kyd, mwandishi wa Kihipania aliyeitumia katika tamthiliya yake ya *The Spanish Tragedie or Hieronimo*, ambaye anasadikiwa kuandika tamthiliya ya *Hamlet*. Baadaye fomula hii ilitumiwa na William Shakespeare, mwandishi maarufu wa tamthiliya nchini Uingereza. Baadhi ya tamthiliya zake zilizotumia fomula hii ni: *Hamlet, Love's Labour's Lost, The Taming of The Shrew* na *A Midsummer Night's Dream* (Klemm, 1966). Baada ya hapo FTT imeendelea kutumiwa na wasanii kadha wa kadha. Ingawa fomula hii ni ya zamani sana, inaendelea kutumiwa kwa sababu ya ubora wake wa kuonyesha msisitizo katika kazi za kisanaa (Zozaya, 1988). Zozaya (keshatajwa), anaongeza kuwa fomula ya tamthiliya ndani ya tamthiliya inamsaidia mwandishi kusisitiza, kupanua na kuzama katika motifu kuu ya kiini cha mchezo; ni mbinu thabiti ya kuifikirisha hadhira kuhusu ubunifu wa maisha halisi na uhalisia wa kazi za ubunifu. Sehemu inayofuata inafafanua namna fomula hii ilivyotumika katika tamthiliya za *Mashetani*, *Giza Limeingia*, na *Kaptula la Marx*.

## 3.0 FTT Katika Tamthiliya Teule za Kiswahili

### 3.1.1 *Mashetani*

Tamthiliya ya *Mashetani* inajadili masuala ya ukandamizaji, kutotenda haki na matabaka yanayosababishwa na tofauti ya kipato katika jamii. Mwandishi anajadili masuala yaliyotokea nchini Tanzania ambayo kimsingi yanafanana kwa kiwango kikubwa na yale yaliyotokea katika nchi nyingi za Kiafrika. Ebrahim Hussein katika tamthiliya hii anamtumia *Shetani* kama *korasi* (Mutembei, 1995) akiwakilisha hasa hulka na sifa za mtu au watu wanaopenda kujineemesha au kujinufaisha kwa kuwanyonya watu wengine. Wakati wa ukoloni, watu wenye sifa hizo walikuwa ni wakoloni na watu walioshirikiana nao. Hata hivyo, baada ya uhuru sifa hizo hasi – sifa za kishetani, zinawaingia viongozi wapya wa Kiafrika. Kwa kuwa sifa hizi ni hulka ya mtu binafsi na watu wengi wana mwelekeo wa kupenda kujinufaisha, mwandishi anasema kuwa watu wengi wana tabia za kishetani, na tabia hizo hujidhihirisha waziwazi pale wapatapo fursa. Hata hivyo, si wote wenye mwelekeo huo. Kwa mfano,

Kitaru, kijana anayetoka katika familia inayostawi kiuchumi kwa njia za kishetani hapendi hali hii ya ushetani na anakerwa na tabia za baba yake ambazo ni za kishetani. Hata kule kuota manyoya katika ndoto ni ishara inayoonyesha kuwa anaelekea kuwa shetani. Hii ni kwa sababu hakuna binadamu mwenye manyoya na mbawa, na mwenye uwezo wa kupaa. Tofauti na Kitaru, Juma, kijana anayetokea katika familia ambayo mali zao zilitaifishwa, ana tabia za ushetani na mawazo yake muda wote yanahusiana na mali. Kwa hiyo, mwandishi anatuambia kuwa nchi ilikuwa na mashetani kabla ya uhuru, na mashetani hayo yanaendelea kutamalaki hadi hivi leo.

### 3.1.2 FTT katika *Mashetani*

Kama tulivyosema hapo juu (Taz. § 1.1) kuwa tamthiliya iliyomo ndani ya tamthiliya nyingine ni sauti ya tamthiliya ilhali sehemu zingine za tamthiliya zilizosalia ni mwangwi. Sehemu hizo, ambazo tunaziita mwangwi, zinafafanua zaidi kile kilichomo katika wazo-kiini, ambalo ni tamthiliya iliyomo ndani ya tamthiliya. Katika *Mashetani,* tamthiliya iliyomo ndani ya tamthiliya nyingine inapatikana katika onyesho la kwanza, sehemu ya kwanza. Wahusika Juma na Kitaru wanacheza mchezo wa kuigiza ambao hadhira ya kwanza, ambayo hatuioni ni wahusika wengine katika tamthiliya, na wasomaji wanakuwa hadhira ya pili. Wasomaji, wanaungana na wahusika wengine, na wanaunda hadhira au dunia halisi iliyoundwa katika mchezo na kuutazama mchezo mwingine.

Shetani anaanza kwa kujitambulisha kuwa ana uwezo wa kutokea katika maumbile mbalimbali na kufanya kila kitu kizuri na kibaya. Shetani anayesemwa hapa ni Mzungu anayekuja kwa sura mbalimbali (Sengo na Kiango, 1975; Nkwera, 1977). Wazungu huja kwa njia ya misaada, mikopo na unyonyaji. Uzungu sio ushetani, ushetani unaozungumzwa hapa ni tabia na hulka ya kinyonyaji. Baadaye roho ya kishetani inamwingia Binadamu ambaye ni Mwafrika. Kifo cha Shetani ni uhuru wa kisiasa wanaopewa Waafrika na kisu kinachotumika ni madaraka. Katika ukoloni, Wazungu walikuwa madarakani, walikuwa na visu vilivyotumika kuwanyanyasia na hata kuwaua Waafrika. Madaraka hayo yaliyoendana na marupurupu waliyopewa viongozi wa Tanzania na nchi nyingine za Kiafrika. Hata hivyo, viongozi wa Tanzania wanahisi kuwa bado hawana uhuru kamili kwa kuwa wanaingiliwa na Wazungu kwa namna mbalimbali. Hii inajidhihirisha pale Binadamu anaposema:

> **Binadamu:** Amekufa. Nimemuua! Nimemuua! Nimemuua, au alitaka nimuue? Umepata kumsikia nani akajichinja mwenyewe? … Alikuwa anacheka huku anakufa! Kuna mtu akacheka huku anakufa? (uk. 8) … Hebu jidhubutu kwanza. Weka akili yako juu ya kitu kimoja – kisu! Kweli kisu kanipa yeye (uk. 9).

Baada ya Wazungu kuondoka, yaani kufa kwa Shetani, viongozi wa Kiafrika wanachukua madaraka wakiwa na matumaini ya kujitupa katika matawi ya miti kama Shetani alivyokuwa akifanya. Tafsiri ya kujitupa huku ni kupata ufahari na starehe zingine za uongozi. Hata hivyo, kunajitokeza matatizo mbalimbali yanayomfanya Binadamu aanguke. Inawezekana ni matatizo ya kiuchumi na yale ya kisiasa yaliyoendelea kutoke nchini Tanzania na sehemu nyingi za Afrika baada ya uhuru. Viongozi wa Kiafrika wanaanza kuhisi kwamba matatizo hayo ya kiuchumi na kisiasa yana mkono wa Shetani ambao ni Wazungu. Binadamu anasema:

> **Binadamu**: … Hukufa! Uko hai! Najua umo humu mtini. Wewe ndiye unayesababisha kuanguka kwangu. Jibu. Unacheka? Nakuhisi unanicheka. … Ninajua ni wewe unayeniangusha. Unaniangusha kisirisiri huku unacheka (uk. 10).

Kipindi kifupi kupita baada ya uhuru viongozi wa Tanzania walianza kujikosoa na wenyewe kuwa huenda lawama nyingi mno zinaelekezwa kwa Wazungu ilhali wao ndio wenye kubadilisha hali duni ya wananchi wao. Hatimaye viongozi wa Tanzania wanaanza kuona kuwa matatizo mengi yanatokana na ulimbukeni na kasumba zilizotokana na ukoloni "yeye katika mimi/yeye-mimi" na hasa zaidi, mifumo ya kikoloni iliyoendelea kutumika katika kuongoza nchi huru. Tamaa ya kutaka kunufaika kwa pupa kama shetani bila kuwa na mipango na usimamizi mzuri wa sera walizojiwekea ndizo zilizosababisha viongozi hao kuona mambo magumu kama inavyojidhihirisha katika tamthiliya:

> **Binadamu**: Kusema kweli, ukija kufikiria hasa, sababu ya kuanguka kwangu ni mimi mwenyewe. Hapana, hasha, siyo yeye katika mimi anayenitaabisha, bali ni mimi-mimi ndiye ninayejiangusha, siyo yeye-mimi (uk. 11).

Hatimaye, Binadamu anaamua kuweka azimio ili kupambana na matatizo yanayomkumba. Inawezekana mwandishi anazungumzia Azimio la Arusha lililolenga kuleta usawa na kuondoa matabaka kinadharia[1]. Mvungi (1978) anadai kuwa azimio la kufanya safari ili kujinasua katika matatizo ni ishara

---

[1] Tamthiliya hii inasawiri vizuri vipindi viwili tofauti. Kipindi cha kwanza ni baada ya kupata uhuru ambapo Watanzania kwa ujumla wake hawakuona matunda ya uhuru kwa sababu wamiliki wa njia kuu za uchumi walikuwa ni walewale lakini wakishirikiana na viongozi wapya wa Kiafrika. Ushetani unaozungumzwa ni ule wa kurithi mifumo na maisha ya kikoloni. Vilevile, tamthiliya hii inaakisi barabara utekelezaji wa Azimio la Arusha ambapo viongozi waliwahadaa wananchi kwa kujilimbikizia mali huku wakihubiri usawa. Wale ambao mali zao zilitaifishwa wakaachwa masikini na mali zao kutumiwa na viongozi kujinufaisha.

kuwa Waafrika wanaamua kujikomboa kimawazo, yaani kuachana na kasumba za kikoloni. Hata hivyo, ni vigumu sana kufanikiwa katika harakati hizi kwa sababu Mwafrika ametawaliwa kwa muda mrefu kimawazo, kiuchumi na kiutamaduni. Matabaka ya kiuchumi yaliyojitokeza baada ya wakoloni kuachia makoloni yao huenda yalichangia katika anguko la Binadamu ambaye anaanguka akijaribu kurukia tawi la mti. Kuanguka huku kunamaanisha wasiwasi na kushindwa kutekeleza malengo na matarajio ya viongozi wa Tanzania. Yumkini kuongezeka kwa matabaka ndiko kunakozua wasiwasi unaoelezwa. Kwa kifupi, haya ni maudhui ya mchezo unaochezwa na wahusika Juma na Kitaru ambao wamevaa uhusika mpya wa Shetani na Binadamu. Hii ndiyo sauti ya tamthiliya hii kama Sengo na Kiango (1975:6) wasemavyo:

> Sehemu hii yenye mchezo Binadamu na Shetani ndio kiini hasa cha mchezo wa *Mashetani*. Sehemu nyingine za kitabu hiki ni za kuendeleza sehemu hii. Hii si kusema kuwa sehemu zote nyingine zilizobaki hazina maana, bali ni kuwa mchezo wote umejengeka katika mchezo huu wa 'Binadamu na Shetani'.

Maonyesho mengine yote yaliyosalia katika tamthiliya hii yanatoa mifano mbalimbali ya hoja za msingi zinazojengwa katika sehemu hii ya mchezo, ndani ya tamthiliya ya *Mashetani*. Maonyesho hayo yanayotoa mifano na ufafanuazi tunayaita *mwangwi*. Sehemu ya pili ya tamthiliya hii inajadili kuhusu migogoro na chuki baina ya familia ya Juma na familia ya Kitaru, na mfadhaiko unaompata Kitaru kutokana na kujilimbikizia mali kwa familia yake. Sehemu ya tatu onyesho la kwanza katika tamthiliya ya *Mashetani* inajadili kuhusu hisia za familia ya Juma kuhusu familia ya Kitaru. Onyesho la pili linajadili kuhusu mtazamo wa watumishi wa Kiafrika, kwa Wazungu na Waafrika, lakini pia, onyesho hili linajadili namna wananchi wanavyoutazama ulimbikizaji wa mali unaofanywa na viongozi wao. Chuki dhidi ya viongozi inawafanya wamfananishe na shetani. Kwa mfano:

> **Mtu 1:** Alaa. Kumbe ndiye huyu? Shetani kweli kweli (uk. 43).

Maisha ya kila siku katika familia hizi mbili, na maeneo mengine yaliyotumika katika tamthiliya hii ikiwemo hotelini, kubadilisha magari kunakofanywa na baba wa mhusika Kitaru, huku shirika lake likifilisika ni miongoni mifano inayoongezea nguvu hoja ya msingi inayoelezwa katika mchezo wa Shetani na Binadamu.

Aidha, onyesho hilo linakamilishwa vizuri na ndoto ya Kitaru. Kimsingi, ndoto ya Kitaru ni sehemu nyingine ambayo wahusika katika tamthiliya wanaletewa mchezo mwingine ambao wanapaswa kuutafsiri huku hadhira halisi pia ikishiriki katika kufumbua mafumbo ya ndoto hiyo. Katika ndoto hiyo, familia

ya Kitaru inaonekana inaingiliwa na sifa za ushetani hali inayomtisha Kitaru. Kuota manyoya na kupaa kunaweza kufananishwa na uwezo wa Shetani kujitupa katika matawi ya mti hali isiyompendeza Kitaru. Ndoto hii inatusaidia kujua kuwa baada ya mashetani, ambao ni Wazungu kuondoka, sasa tuna mashetani Waafrika. Kwa ujumla tunaweza kuhitimisha sehemu hii kwa kusisitiza kuwa matumizi ya FTT katika *Mashetani* yanaonyesha wazo kuu – sauti, ambapo sehemu zingine zilizosalia ni mwangwi wa sauti hiyo.

### 3.2 *Kaptula la Marx*

Tamthiliya ya *Kaptula la Marx* inajadili hali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii baada ya Azimio la Arusha. Tunaweza kusema ni mwendelezo wa tamthiliya ya *Mashetani*. Tamthiliya ya *Mashetani* na *Kaptula la Marx* zinafanana kwa kiasi kikubwa kimaudhui na kifani. Zote zinahusu changamoto za kisiasa na kiuchumi katika nchi huru zilizotoka kutawaliwa. Kama ilivyo katika *Mashetani,* maudhui ya tamthiliya hii yanaakisi sio tu nchi ya Tanzania, bali changamoto za kisiasa na kiuchumi zinazozikabili nchi mbalimbali za Kiafrika (Wamitila, 2000). Mwandishi anaonyesha unafiki wa viongozi katika nchi inayofuata siasa ya ujamaa na kujitegemea. Mawaziri na wabunge hawatimizi majukumu yao iwapasavyo, yaani kuishi na kutekeleza sera ya ujamaa, badala yake wanamwaminisha kiongozi wao kuwa hawatamwangusha lakini matendo yao hayasadifu kile wasemacho. Usaliti unafanywa na viongozi ambao waliaminiwa sana na kiongozi wao, rais Kapera. Mfano mzuri ni ule unaoonyesha kuwa rais Kapera anafikiria kumwoa waziri ambaye anamgeuka na badala yake anaandaa njama za kumpindua.

#### 3.2.1 FTT katika *Kaptula la Marx*

Tamthiliya inayopatikana ndani ya *Kaptula la Marx* imo katika onyesho la tatu, kati ya maonyesho sita. Sehemu hii inawahusisha wahusika wafungwa ambao wanavaa uhusika mwingine na kutufanya hadhira tuingie katika tamthiliya nyingine. Wafungwa wanacheza tamthiliya tatu tofauti zinazofungamana kimaudhui ambazo ni: bungeni, kwenye maandamano, na mahakamani. Sehemu ya bunge inaonyesha kipindi cha maswali na majibu kama ilivyo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Bila shaka sehemu hii inaonyesha kuwa wabunge na mawaziri hutumia muda mwingi kujadili masuala yasiyo na tija kwa taifa kama inavyojidhirisha katika mfano ufuataao:

> **Mfungwa 1:** Ndugu Spika swali la nyongeza! Ndugu Waziri anaweza kutueleza wanyama wa porini wanakoga mara ngapi? Wangapi wanakula majani na wangapi wanakula wanyama wenzao na mwisho wangapi wanakula sisimizi na mchwa? (*Makofi kutoka kwa wabunge)*(uk. 14).

Aidha, kwa mbunge kuanza na swali la nyongeza inaonesha kuwa maswali ya wabunge wengi si ya msingi. Baada ya swali hilo kunatokea fujo huku kila mbunge akitaka kuuliza swali la nyongeza bila utaratibu. Tamthiliya hiyo ya bunge inaishia hapohapo. Baada ya hapo, wafungwa wanaamua kuigiza kitu kingine. Mwandishi anaona changamoto kubwa katika kipindi hiki ilikuwa ni ujenzi wa jamii mpya na sera ya ujamaa. Wabunge walipaswa kujadili mafanikio, vikwazo na changamoto katika utekelezaji wa sera hiyo badala ya kujadili masuala yasiyohusiana na sera ambayo inaongoza nchi. Wakati kila mbunge akitaka kuuliza swali la nyongeza bila utaratibu, Mfungwa 6 alikuwa ametulia. Kutulia huko kwa Mfungwa 6 ni msisitizo unaoonyesha kuwa watu makini wanaoelewa masuala mbalimbali hawashiriki katika mivutano ambayo haina umuhimu katika maendeleo ya taifa.

Baada ya tamthiliya ya bunge kusitishwa, wafungwa wanaamua kuandamana ili kutoa hisia zao kwa viongozi wa Afrika, ambapo maandamano hayo yanahitimishwa kwa kusoma risala. Mwandishi anatuambia kuwa ingawa maandamano ni haki ya kila raia katika kuunga mkono au kupinga masuala kadha wa kadha, yanapofanyika dhidi ya serikali yanachukuliwa kuwa ni makosa. Raia wananyimwa haki yao ya kuandamana. Wafungwa wanaamua kuandamana ili kuonesha na kusisitiza kuwa maandamano ni haki ya msingi. Hii inadhihirishwa pale Mfungwa 6 anaposema:

> **Mfungwa 6**: Acheni fujo! Tuache majadiliano. Maswali yenu ni mengi mno! Huko nje hakuna tena maandamano. Watu wanapigwa mabomu ya machozi (uk. 14).

Maandamano yanaanza kufanyika huku baadhi ya maneno kadha wa kadha yanayoonesha sababu za maandamano hayo ikiwa ni pamoja na chuki mbalimbali dhidi ya viongozi wa serikali kama ifuatavyo:

> **Mfungwa 4**: Tuandambane basi! Tumechoka kudanganywaaaaaa!
> **Wote**: Tumechoka kudanganywa!
> **Mfungwa 4**: Tumechoka kuchezewa!
> **Wote**: Tumechoka kuchezewa!
> **Mfungwa 4**: Mchakamchaka!
> **Wote**: Chinjaaa!
> **Mfungwa 4**: Wabunge wote!
> **Wote**: Chinjaaa!
> **Mfungwa 4**: Mawaziri wote!
> **Wote**: Chinjaa! (uk. 14).

Maneno hayo yanaonesha chuki waliyonayo watu dhidi ya viongozi wao kutokana na kutoridhishwa na utendaji wao. Tunaelezwa katika maandamano

hayo kuwa hata Mfungwa 6 anashiriki ipasavyo.[2] Mwandishi anaonesha kuwa masuala yanayosemwa katika maandamano hayo ni ya msingi ikilinganishwa na yale yaliyokuwa yakijadiliwa bungeni. Maandamano hayo yanakamilishwa kwa usomaji wa risala. Risala hiyo inalaani vitendo vya ukandamizaji vilivyofanywa na jeshi la polisi katika kusimamisha maandamano ikiwa ni pamoja na kuwapiga waandamanaji na baadhi yao kuwashikilia. Aidha, risala hiyo inagusia kichocheo cha maandamano hayo ambacho ni kujiongezea mishahara na marupurupu kwa viongozi na kuwaacha watu maskini kama wakulima na wafanyakazi katika lindi la umaskini. Mwisho, maandamano hayo yalilenga kuonesha kutowaamini viongozi wa serikali katika kushughulikia kero zinazowakabili wananchi. Kama inavyoelezwa katika tamthiliya hii:

> Maandamano yetu yalikuwa ya amani, na hakuna hata mmoja wetu aliyekuwa na silaha ya aina yoyote. … lakini polisi walituvamia kwa unyama mkubwa. Wengi wetu, wakiwemo akina mama, wameumia vibaya kutokana na ukatili wa polisi. Tunalaani ukatili huu wa polisi. … Maandamano haya tuliyapanga ili kupinga vitendo vya viongozi wa nchi … mawaziri na wabunge wao kujiongezea mishahara mikubwa na marupurupu wakati wananchi wao wamo katika shida nyingi! … masilahi ya wakulima na wafanyakazi … hayawezi kutetewa na viongozi, mawaziri au wabunge (kur. 15, 16).

Sehemu ya mwisho ya tamthiliya hii inajadili suala la haki, kama mwandishi asemavyo:

> **Mfungwa 6**: … Huko nje hakuna tena haki!
> **Mfungwa 5**: Isipokuwa humu jela!
> **Mfungwa 4**: Na tuionyeshe basi hiyo haki. (uk. 14).

Mwandishi analigusia suala la haki katika jamii iliyojitangazia kuwa inaishi kijamaa. Mahakama katika nchi za kijamaa, zinapaswa kutenda haki zaidi kwa sababu hakuna matabaka yaliyobainishwa wazi katika jamii. Lakini mwandishi anaonesha unafiki wa jamii yenyewe kwa sababu mhimili mmoja kati ya mihimili yake muhimu inayotazamiwa kutenda haki bila kuendeleza matabaka; inatenda kazi zake kinyume na maadili. Mwandishi anaonesha mwizi wa mkate katika duka la Mhindi akifungwa jela miaka 10 na viboko 25 huku mtu aliyeliibia shirika la ndege kiasi cha shilingi milioni 21 anafungwa jela kwa siku moja kama inavyodhihirika katika mfano huu:

---

[2] Wamitila (2000) anadai kuwa kilichomchochea mwandishi kuandika tamthiliya hii ni maandamano yaliyofanywa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya tarehe 5 Machi 1978, kupinga viongozi kujiongezea marupurupu, kinyume na misingi ya Azimio la Arusha. Kama hiki ni kichocheo cha maandamano hayo, bila shaka maandamano hayo yalizimwa kwa nguvu na jeshi la polisi.

| | |
|---|---|
| **Mfungwa 1**: | Huyu anashitakiwa kwa kosa la kuiba pesa za shirika la ndege, kiasi cha shilingi milioni ishirni na moja! |
| **Mfungwa 6**: | Unakiri kosa! |
| **Mfungwa 3**: | Ndiyo, nakiri. |
| **Mfungwa 6**: | Jela kwa muda wa siku moja! (Wengine wote wanacheka na kuzomea. Hata Namba 1 ambaye ni polisi, pia Namba 4 ambaye ni meza) wanazomea. Mnachekacheka nini? Wote jela! (Anampiga teke Namba 4) Wote *contempt of court!* (kur. 16, 17). |

Katika sehemu hii mwandishi anasisitiza kuwa haki haitendeki. Watu wasio na uwezo wanaadhibiwa zaidi kuliko watu wenye uwezo. Ingawa siasa ya ujamaa inalenga kuimarisha usawa na maendeleo ya jamii yote kwa ujumla, hali halisi ni tofauti. Bado jamii haizingatii misingi mikuu ya kijamaa kwa sababu mwenye pesa anathaminiwa zaidi ya maskini. Onyesho la tatu la tamthiliya hii kimsingi ndio sauti ya tamthiliya yenyewe; maonyesho mengine ya tamthiliya hii yaliyosalia ni mwangwi wa sauti hii kwa sababu yanafafanua na kutoa mifano zaidi.

Maonyesho mengine ya tamthiliya hii yanajadili mifano kadha wa kadha ya onyesho la tatu ambalo linajadili kwa kina matatizo mbalimbali yaliyojitokeza nchini Tanzania hasa utekelezaji wa siasa ya ujamaa. Sehemu nyingine za tamthiliya hii kama vile onyesho la kwanza, zinadokeza changamoto za jumla katika nchi huru kama vile matatizo ya kiuchumi, kisiasa, na hali ngumu za wakulima na wafanyakazi. Kwa mfano, onyesho la pili, linaonesha rais Kapera akijadiliana na mawaziri wake, ambapo mjadala mkubwa hauhusu changamoto zinazowakabili wananchi, badala yake wanasifia kitendo cha kuukumbatia ujamaa ilhali wao wenyewe hawauamini wala kuufuata. Onyesho la nne linajadili changamoto za utekelezaji wa siasa ya ujamaa, mustakabali na nafasi ya watu wa chini kama wakulima na wafanyakazi katika utekelezaji wa sera hiyo.

Kwa hiyo, tamthiliya inayoonyeshwa na wafungwa ndiyo kiini hasa cha tamthiliya hii ikijadili matatizo yote ya msingi katika nchi huru ambayo ni uvunjaji wa haki za kibinadamu unaofanywa na serikali, uongozi mbovu ikiwa ni pamoja na wabunge na mawaziri kushindwa kujadili masuala ya msingi. Tatizo la unafiki wa mawaziri na hali ngumu ya maisha ya watu wa chini yanatolewa mifano kama mwangwi wa kiini kikubwa cha matatizo ambayo ni kukosa viongozi wanaojali mawazo ya wananchi, na badala yake wanawaendesha wananchi katika nchi huru kama wafungwa wa kifikra na kimaumbile.

### 3.3 *Giza Limeingia*

Hii ni tamthiliya inayojadili tatizo la vijana kukimbilia mijini wakiwa na matumaini ya kupata kazi. Baada ya kukosa kazi vijana hawa ambao wamesoma na ambao hawajasoma, ama wanajishughulisha na vitendo vya kihalifu, kwa upande wa vijana wa kiume au wanashawishiwa kufanya rushwa ya ngono kwa matarajio ya kupata kazi, kwa upande wa vijana wa kike. Athari zake ni kukamatwa na kuwekwa ndani au kuuawa kwa wale wanaojishughulisha na uhalifu ilhali wasichana wanapata ujauzito na baadaye kuwa na watoto wanaoshindwa kuwalea. Hata hivyo, mwandishi anadokeza mipango duni ya kuwaendeleza vijana vijijini na tatizo linalochangia vijana kukimbilia mijini.

### 3.3.3 FTT katika *Giza Limeingia*

Tamthiliya ndani ya tamthiliya hii inapatikana katika sehemu ya kwanza ambapo mhusika Kopa, kijana anayejishughulisha na uuzaji wa karanga, utapeli na wizi, anaigiza na Mashaka, kijana aliyemaliza kidato cha nne lakini hana kazi. Kopa anavaa uhusika wa Msichana na Mashaka anavaa uhusika wa Meneja. Katika tamthiliya hii, msichana anaomba kazi lakini meneja anadai kuwa hakuna kazi. Hata hivyo, Meneja anamwambia Msichana kuwa yupo tayari kumwachisha kazi mtu mwingine na nafasi yake ichukuliwe na msichana huyo, na msichana anashinikizwa kushukuru kabla ya kupatiwa kazi. Kushukuru kunakozungumziwa hapa ni kutoa rushwa ya ngono kama inavyojidhihirisha katika sehemu ifuatayo ya tamthiliya hii:

| | |
|---|---|
| **Mashaka**: | Naweza kutumia madaraka yangu, nikamfukuza mfanyakazi mmoja, … naweza nikamstaafisha mfanyakazi wa kiwanda hiki … halafu sehemu yake nikakuajiri wewe. Unaelewa? |
| **Kopa**: | Ndiyo Meneja, nitashukuru sana. |
| **Mashaka**: | Utashukuru! … Unajua kushukuru? |
| **Kopa**: | Najua Meneja. |
| **Mashaka**: | Lazima ushukuru kabla, sio baada ya kupata kazi. |
| **Kopa**: | Ndiyo mzee. |
| **Mashaka**: | Unaelewa lakini lugha yangu? |
| **Kopa**: | Ndiyo Meneja naelewa (uk. 17). |

Hiyo ni tabia ya mameneja wengi wasio waadilifu wanaosimamia ofisi za serikali kwa manufaa yao. Sehemu hii inaonesha kwamba kuna upendeleo mkubwa wa ajira katika makampuni na mashirika ya umma.

Tamthiliya nyingine ndani ya tamthiliya inapatikana katika sehemu ya pili ya *Giza Limeingia.* Katika sehemu hii Kopa, Mashaka na Salome, wahusika wa tamthiliya hii, wanaigiza kama Waziri, Mwandishi wa Habari na Mwenyekiti wa Kijiji. Katika sehemu hii, Mwenyekiti wa kijiji anamtembeza Waziri katika

miradi mbalimbali inayofanywa chini ya serikali ya kijiji. Mwandishi anaonyesha uzalishaji usio na tija katika shughuli za kilimo kiasi cha kukatisha tamaa kama mfano ufuatao unavyoonyesha:

**Salome:** Hili ndilo shamba letu la mpunga. Kuanzia kulee… hadi kule.
**Kopa:** Ndiyo ndiyo. Maendeleo makubwa haya.
**Salome:** Mwaka jana tulivuna magunia arobaini ya mpunga.
**Mashaka:** Kama ni hivyo ndugu waziri, huwezi kuita haya ni maendeleo.
**Kopa:** Kwa nini ndugu mwandishi wa habari.
**Mashaka:** Ekari moja gunia nne tu! Hayo si maendeleo, shamba lingetunzwakitaalamu ekari moja ingebidi itoe gunia nane hadi kumi, sio nne tu (uk. 76).

Mwandishi anaendelea kusisitiza kuwa mali nyingi za umma kama vile matrekta yaliyopelekwa vijijini hayakudumu, yaliharibika na kutelekezwa kwa sababu wanakijiji hawakuandaliwa kufanya matengenezo pindi vifaa hivyo vinapoharibika. Vilevile, mwandishi anasisitiza zifanywe jitihada za makusudi za utafutaji wa masoko ya mazao na zana za mikono zinazotengenezwa na vikundi vya vijana. Kwa kifupi mwandishi anadai kuwa serikali haikuandaa mpango mzuri wa kuleta maendeleo vijijini. Sera nyingi zilizingatia misukumo ya kisiasa badala ya utaalamu wa kiuchumi. Matokeo ya mipango hiyo duni ni vijana kukimbilia mijini wanakotumaini kupata ahueni ya maisha.

Kwa hiyo, tamthiliya mbili ndani ya *Giza Limeingia* ni sauti ambayo inakamilishwa na mwangwi katika sehemu nyingine zilizosalia. Maeneo mengine ya tamthiliya hii yanaonyesha vijana wa kijijini wanavyokabiliana na ugumu wa maisha, operesheni ya kuwaondoa wazururaji na kuwapeleka vijijini ili wakajishughulishe na uzalishaji mali badala ya kupoteza muda mjini. Halikadhalika, sehemu nyingine zinaonyesha mhusika Kopa anavyomshawishi Mashaka ashiriki katika vitendo vya uporaji ili wajipatie kipato, lakini kabla hawajatekeleza mpango huo, Kopa anapigwa risasi katika uhalifu na inaelekea alifariki dunia. Kwa kifupi, tamthiliya ndani ya *Giza Limeingia* ndicho kiini hasa cha tamthiliya hii.

## 4.0 Dhima na Sababu ya Matumizi ya FTT katika Tamthiliya Teule

Matumizi ya FTT katika tamthiliya teule yametumika kwa namna kuu mbili. FTT katika tamthiliya za *Mashetani* na *Kaptula la Marx* imetumika kama kiini kijengacho tamthiliya yote ambapo sehemu za tamthiliya zilizosalia zimefafanua na kutoa mifano kadha wa kadha kuhusu mada inayojadiliwa katika kitabu. Katika tamthiliya ya *Giza Limeingia,* FTT imetumika kama wazo kiini lakini ikielezea zaidi chanzo cha tatizo linalojadiliwa katika tamthiliya nzima. Sehemu kubwa ya tamthiliya hii inaelezea zaidi matokeo ya mipango

mibovu na upendeleo wa ajira, tatizo linalojadiliwa katika tamthiliya ndani ya tamthiliya.

Matumizi ya FTT humuwezesha mwandishi kupanua wigo wa matukio, na hiyo husaidia katika kujenga maudhui, pasipo kuongeza wahusika wengine wala kubuni mandhari mapya. Matumizi ya FTT katika tamthiliya teule zote tulizoziona yamepanua wigo wa matukio kisanaa na kufanya maudhui ya kazi hizi yaeleweke vizuri.

Sababu nyingine kubwa inayochangia matumizi ya fomula hii ni kuonyesha uhusiano na mitazamo waliyonayo wahusika na uhusika wao kuhusu masuala muhimu yanayojadiliwa katika tamthiliya. Kwa kawaida, uhusiano huo una umuhimu mkubwa katika kujenga dhamira za tamthiliya mahsusi. Kwa mfano, katika *Giza Limeingia* baada ya kutoka Gezaulole na kupata taarifa kuwa mjini hakuna kazi, kazi zipo vijijini, Salome anaigiza kama mwenyekiti wa kijiji akionyesha mafanikio makubwa na kudai kuwa inawezekana kuishi kijijini. Kwa upande mwingine, Mashaka, kijana asiyeamini kuwa kuna uwezekano wa kuishi vizuri kijijini, aliigiza kama mwandishi wa habari aliyekuwa akidadisi kila kisemwacho na Salome (Mwenyekiti wa kijiji). Mwelekeo wa aina hiyohiyo unajitokeza katika mchezo wa Msichana na Meneja ulioigizwa na Kopa na Mashaka, ambapo Kopa alikuwa akiamini kuwa wasichana hutoa rushwa ya ngono ili kupata kazi. Suala hili lilipingwa na Mashaka. Misimamo hiyo inajionyesha wazi pale Mashaka anapobaini kuwa tamthiliya hiyo inaelekea kueleza ukweli kuhusu mpenzi wake Salome, na kumfanya asiendelee kuigiza mchezo huo. Uhusiano wa aina hiyo unajitokeza pia baina ya Juma na Kitaru katika *Mashetani* ambapo kunatokea ubishi kuhusu kubadilishana uhusika wa nani acheze nafasi ya Shetani na nani Binadamu, hasa baada ya tofauti zao kifikra kuanza kuonekana bayana.

## 5.0 Hitimisho

Kwa kawaida mwandishi hafungwi kutumia mtindo fulani katika tamthiliya yake. Mifano mbalimbali ya utunzi wa tamthiliya za kipekee zimeelezwa vizuri na Senkoro (keshatajwa). Yumkini mitindo mingine mingi itaendelea kujitokeza kulingana na ubunifu wa watunzi wa tamthiliya. Hata hivyo, matumizi ya FTT yanaonekana kuwa ni mbinu mojawapo kati ya mbinu nzuri katika uandishi wa tamthiliya. Ndio maana pamoja na kutumika kwa karne kadhaa lakini bado inapendelewa na waandishi maarufu wa tamthiliya, hususan tamthiliya za Kiswahili. Pamoja na kuwa na dhima na kutumiwa kwa namna tofautitofauti na waandishi, matumizi ya FTT si ya kiholela, badala yake, utumizi wake una dhima kubwa kimaudhui na kimtindo. Utumizi wa FTT na dhima zake vinapaswa kuchunguzwa zaidi katika tamthiliya na kumbo nyingine za fasihi kama vile riwaya.

## Marejeo


Hussein, E.N. (1971). *Mashetani.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Kezilahabi, E. (1996). *Kaptula la Marx.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Klemm, E.G.B.A. (1966). *Play Within Play in Shakespeare's Comedies.* Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Jimbo la Ohio.

Mbogo, E. (1980). *Giza Limeingia.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mlama, P. (1983). "Utunzi wa Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania". Katika *Makala za Semina ya Waandishi wa Kiswahili III. Fasihi. TUKI* kur. 206-225.

Mulokozi, M.M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mutembei, A. K. (1995). Korasi na Uhusiano wake na Sanaa za Maonyesho: Uchambuzi wa Kidayakronia. *Kioo cha Lugha.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kur. 67-73.

Mvungi, T. (1978). "Mashetani" na Mwamko wa Siasa. Katika *Mulika na. 13.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Kur. 16-20.

Nkwera, F. (1977). "Ebrahim N. Hussein: Mwandishi wa Michezo ya Kuigiza". Katika *Mulika Na. 11.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. *Kur. 38-46.*

Sengo, T.S.Y. na S.D. Kiango, (1974). *Ndimi Zetu: Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili 2.* Dar es Salaam: Longman.

Senkoro, F.E.M.K. (2006). "Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi". katika *Kioo cha Lugha.* Dar es Salaam: Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kur. 22-38.

Theatre. (2012). In *Encyclopædia* Britannica. katika http://www.britannica.com/EBchecked/topic/590186/theatre. Iliyosomwa tarehe 8 Machi 2012.

Van Peer, W. na F. Hakemulder, (2006). "Foregrounding". Katika *The Pergamon Encyclopaedia of Language and Linguistics, mh. Keith Brown.* Oxford: Elsevier, Juz. 4, kur. 546-551.

Wamitila, K.W. (2000). Umatinishaji wa Historia na Historia ya Umatinishaji: Kaptula la Marx (E. Kezilahabi). *Mulika Na. 26* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. *kur. 1-8.*

____________ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Books.

Zozaya, P. (1988). Plays-within-Plays in Three Modern Plays: Michael Frayn's Noises Off, Tom Stoppard's The Real Thing and Alan Ayckbourn's A Choras of Disapproval. Katika *Revista Alicantina de Estudios Ingleses, Na. 01. uk.`. 189 -201.* Katika <http://rua.ua.es/dspace/bitstream/10045/5584/1/RAEI_01_14.pdf> Ilisomwa tarehe 8 Machi 2012.